



Ministry of Environment
and National Resources

KUHUSIANA NA NOTISI ILYOCHAPISHWA KATIKA GAZETI RASMI LA SERIKALI KUHUSU KUPIGWA MARUFUKU MIFUKO YA PLASTIKI



nema
mazingira yetu | uhai wetu | wajibu wetu
National Environment
Management Authority

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA (FAQs)

AINA YA MIFUKO YA PLASTIKI ILIYOPIGWA MARUFUKU KUPITIA ILANI YA GAZETI RASMI LA SERIKALI



1

Mifuko ya kubebea bidhaa

Bila kuzingatia unene, wembamba au rangi mifuko hii ya plastiki hutumika katika maduka ya Supermarket, maduka ya rejareja, majengo ya kibiashara, maduka ya mboga, matumizi ya kawaida nyumba na shughuli nyinginezo.



2

Mifuko laini

Aghalabu hutumika katika maduka ya kuuza mboga na yanajumuisha yale ambayo hutumika kubebea takataka.

SWALI 1: Ni Mifuko ipi ya plastiki imepigwa marufuku?

JIBU : Inahusisha mifuko yote ya plastiki inayotumika kubebea au karatasi nyembamba za kufungia bidhaa za kibiashara au kwa matumizi ya nyumbani.

SWALI 2: Mfuko wa plastiki wa kubebea bidhaa ukoje?

JIBU : Huu ni mfuko wa plastiki unaotumika mara kwa mara na una sehemu ya kushikia juu kwa mfano angalia picha ya kwanza juu.

SWALI 3: Karatasi za plastiki nyembamba ni ipi?

JIBU : Huu ni mfuko usiokuwa na sehemu ya juu ya kushikia kwa mfano angalia picha ya pili juu.

SWALI 4: Nini kilichosababisha mifuko ya plastiki kupigwa marufuku?

JIBU : Kwa kawaida mifuko ya plastiki hutengenezwa kwa ajili ya matumizi ya mara moja tu na kisha kuharibika na kutupwa baada ya kutumika. Mifuko hiyo inapeperushwa na upepo kwa urahisi na miongoni mwa takataka zilizorundikana kando ya barabara, kingo za mito, fukwe za maziwa au majalalani. Mifuko ya plastiki inatengenezwa kutokana na mafuta na gesi za kiasili, hivyo haziozi na husalia ardhini kwa muda mrefu zinapofukiwa.

SWALI 5: Je, mifuko ya plastiki inayotumiwa viwandani kufunga bidhaa pia imepigwa marufuku?

JIBU : La hasha. Marufuku haijumuishi mifuko inayotumiwa viwandani kufunga bidhaa, almradi iwe imetimiza viwango vya ubora vilivyowekwa na haiuzwi au kutolewa bure kwa wateja viwandani. Aidha, mifuko hiyo ni sharti iwekwe alama ya chapa ya kiwanda kinachotengeneza bidhaa husika.

SWALI 6: Je, siku ya mwisho ambayo watengenezaji na waagizaji wa bidhaa wanafaa kukoma kuwapa wateja wao mifuko ya plastiki ni ipi?

JIBU : Siku ya mwisho ya kuwapa wateja mifuko ya plastiki ni Agosti 28, 2017. Baada ya hii, watengenezaji na waagizaji wa bidhaa wanastahili kuripoti kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA) kuhusu kiasi cha karatasi zilizosalia bila kutumika ili hatua madhubuti zichukuliwe.

SWALI 7: Je, viwanda vinavyotengeneza mifuko ya plastiki ya kuuza nje ya nchi vitaendelea kuitengeneza?

JIBU: La hasha. Utengenezaji wa karatasi za plastiki utafikia kikomo Agosti 28, 2017.

SWALI 8: Je, kutakuwa na muda zaidi wa kipindi cha neema kwa wafanyabiashara kuanza kutekeleza marufuku hiyo?

JIBU: Noti katika Gazeti Rasmi la Serikali ilichapishwa mnamo Februari 28, 2017 kwa lengo la kuruhusu kipindi cha neema cha miezi sita (6) kabla ya kuanza kutekelezwa Agosti 28, 2017.

SWALI 9: Je, wafanyabiashara na wenye maduka wataruhusiwa kuendelea kutumia mifuko ya plastiki watakayosalia nayo baada ya makataa ya Agosti 28, 2017?

JIBU: Hapana. Wafanyabiashara, wakiwemo wenye maduka, wanastahili kutumia mifuko yote ya plastiki iliyosalia katika kipindi hiki cha neema kabla ya makataa. Baada ya makataa, wenye maduka na wafanyabiashara wengineo watatakiwa kuwasilisha ripoti kwa NEMA kuhusiana namifuko iliyosalia ili hatua mwafaka zichukuliwe.

SWALI 10: Je, wafanyabiashara wanaweza kutumia mifuko ya karatasi za kawaida badala ya mifuko ya plastiki kuwafungia wateja bidhaa?

JIBU : Ndiyo.

SWALI 11: Je, ni mifuko ipi ya karatasi za kawaida inayofaa kutumiwa badala ya mifuko ya plastiki?

JIBU : Mifuko mbadala inajumuisha, mifuko iliyotengenezwa kwa karatasi za kawaida, nguo, vikapu, mifuko iliyotengenezwa kwa nyuzi za mikonge na mifuko na begi wanazokuja nazo wateja.

SWALI 12: Ni maduka yapi yameathiriwa na marufuku hiyo?

JIBU: Maduka na wafanyabiashara wote.

SWALI 13: Je, Wafanyabiashara wadogo wanaouza bidhaa za rejareja wanaruhusiwa kutumia karatasi za plastiki?

JIBU: La hasha.

SWALI 14: Je, marufuku hiyo inazuia uuzaji wa karatasi za plastiki zinazotumika kubebea takataka?

JIBU: Ndiyo.

SWALI 15: Je, maduka ya kuuza nguo yameruhusiwa kutumia mifuko ya plastiki baada ya tarehe 28 Agosti, 2017?

JIBU: Hapana. Wanaoruhusiwa kutumia karatasi hizo ni viwanda vya kutengeneza bidhaa ambavyo ni sharti vitumie karatasi zilizoidhinishwa kama ilivyoielezwa katika swali la tano (5).



ISO 9001-2008 Certified

✉ dgnema@nema.go.ke

www.nema.go.ke

Facebook National Environment Management Authority - Kenya

Twitter @NemaKenya

YouTube NemaKenya

Ripoti matukio na malalamiko kwa: 0786 101 100

Mazingira Yetu, Uhai Wetu, Wajibu Wetu



TOWARDS A GLOBALLY COMPETITIVE AND PROSPEROUS NATION